EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

BBN Limited TZA

# OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA UTOAJI WA Bidhaa za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT), Elektroniki.

## REF ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0112

BESIX Ballast Nedam Limited, inayotekeleza Huduma za awali za ujenzi wa Gati na Kituo cha Kupakia Mafuta katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni ya kitaalamu kueleza nia yao kwa utoaji wa huduma ya Ugavi wa:

**- Vitu vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, ununuzi wa vifaa vya kielektroniki**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha uhandisi, ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya bomba la kusafirisha mafuta ghafi linalovuka Uganda na Tanzania ikijumuisha. Gati yenye Kituo cha Kupakia Mafuta kwenye Meli za Mafuta, karibu na Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA UPEO WA VIFAA / HUDUMA:**

- Ugavi wa vifaa vya elektroniki vya ofisi
- Mashine za kupiga chapa (printer) / kutoa vivuli (copier) / skena au kisoma maandishi (Scanner)
- Vifaa / Vitu vya teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT)

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**

Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa:

- Wasifu wa kampuni na uthibitisho wa rasilimali za kutosha za kifedha na zenye uwezo.
- Uthibitisho wa Cheti au Hati Safi ya Mlipa kodi ya Kampuni
- Orodha ya tajriba iliyo na historia ya ugavi husika / rekodi inayoonyesha uzoefu usiopungua miaka mitano (5) katika ugavi na uuzaji wa bidhaa zinazohitajika za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) kulingana na viwango vya kimataifa vinavyojulikana katika biashara ya Mafuta na Gesi au soko linalolinganishwa.
- ISO 9001:2015, ISO 14001:2015
- Kuzingatia kanuni za mafuta ya petroli za matumizi ya rasilimali za ndani (Local Content) ya 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Wasambazaji na Watoa Huduma wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha maombi, unapendekezwa sana.
- Orodha ya vifaa pamoja na modeli / chapa/ tovuti ya mtandao unaozitangaza/shiti za kiufundi (technical sheets).

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji na yana uwezo wa kutoa huduma yanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu barua pepe kwa **procurement@bbnltd.co.tz (Ukubwa wa Barua Pepe na viambatanishi: 20 MBs & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya tarehe **17 Februari 2023 , 1800hrs** Saa za Tanzania.

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji ya chini zaidi yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka :** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.